

*Meli kubwa ya uvuvi kuleta fursa *

Na Moshi Lusonzo

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amesema Tanzania itanufaika kwa kuingiza shilingi bilioni moja kila mwaka na tani 300 za samaki, baada ya meli kubwa ya uvuvi wa bahari kuu kuanza kufanya kazi.

Akizungumza wakati akipokea meli hiyo inayoitwa Pacific Star inayomilikiwa na kampuni ya Al Bacora Group, katika Bandari ya Dar es Salaam, Waziri

Ndaki alisema faida hiyo inatokana na serikali kuamua kufungua milango kwa wawekezeji wakubwa katika sekta ya uvuvi.

Alisema katika makubaliano hayo, kampuni hiyo inayomilikiwa na rasi wa Hispania, itapewa leseni ya uvuvi na kupeperusha bendera ya Tanzania, itatoa masunzo ya uvuvi kwa Watanzania watano na kujenga kiwanda cha kuchakata samaki nchini.

Waziri huyo alisema meli hiyo ya kisasa yenye uwezo wa

kubeba tani 2,000 za samaki kwa mkupuo minioja, itashughulika na uvuvi wa samaki wa aina ya Jodari na aina 100 zingine kila baada ya miezi minne, hivyo itapunguza pengo la ukosefu wa samaki.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuamua kufungua milango kwa wawekezaji wakubwa wa uvuvi kufanya kazi nchini kwetu, mell lititupata faida kubwa za kuchumi na hapa tumeanza kwani meli zingine zinakuja," alisema.

Alisema katika mgawanyo wa

mazao ya samaki, kampuni hiyo itatoa tani 200 za samaki aina ya Jodari na aina 100 zingine kila baada ya miezi minne, hivyo itapunguza pengo la ukosefu wa samaki. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Suleiman Masoud Makame, alisema serikali zote mbili zina matumaini chanya na meli hiyo kwa sababu italeta mapinduzi mapya ya uvuvi baharini.

"Natarajia kila kitu kilichomo kwenye makubaliano kitakele-

zwa kwa ukamilifu ili kila upande unufaika na rasilimali ya bahari, serikali zote mbili zinataka sekti ya uvuvi iwe uti wa mgogo wa uchumi wetu," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Dk.Christina Ishengoma, alipongeza serikali kupitia Taasisi yake ya Bahari Kuu, kipatia leseni kampuni hiyo kuvua samaki kwani itasaidia wananchi kupata chakula hicho kwa bei naftu.

Mhasibu

KUCHUKU! Irdi mawazo hii uapua ya kumkamata Oktoba 20, mwaka jana, akiwa katika nyumba ya kulala wageni ya Sadina mkoani Mtwara.

Baadhi ya vijana wa Kanisa la Waadventista Wasabato la Mbezi Luis, mkoani Dar es Salaam, wakichangia damu katika Hospitali ya Taifa Muhimili-Mloganzila, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Matendo ya Huruma ya kanisa hilo, juuji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

*UDSM kuanza uzalishaji wa vifaranga

Na Christina Mwakangale

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imewekeana salini na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) utekelezaji wa ujenzi na uendeshaji wa Kituo cha Taifa cha Rasilimali za Ukuza (Viumbe Maji Bahari (NMRC), unaanza kwa awamu ya kwanza kwa gharama ya Sh. Bil 1.59.

Kituo hicho kinatatajla ku-zalisha samaki, kamba miti, kaa, majongoo bahari, chaza kwa tani zipatazo milioni moja hadi 2.5.

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Rashid Tamatamah, aliyasema hayo jana katika mradi huo una-jengwa kwenye kampasi ya Kunduchi Shule ya Sayansi ya

Teknolojia ya Uvuvi (SOAF) kupitia Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) na Benki ya Dunia (WB).

Alisema yapo mahitaji makubwa nchini ya vifaranga vya samaki pamoja na chakula chao na kwamba uzalishaji hauendani na mahitaji, alisema mwaka 2020/21 jumla ya vitotoleshi 33 vitotolesha vifaranga milioni 22 huku hali halisi ya mahitaji ni milioni 115.

"Kituo hiki na vingine ni muhimu kwenye huduma za ukuza ugani, viumbe hai baharini kuunda na kutengeneza botti, kushona nyavu, kuzalisha vifaranga na vyakula vya samaki, kutengeneza vizimba na blashara ya samaki. Samaki

huchangia takriban asilimia 30 ya protini inayotokana na wan-yama," alisema Dk. Tamatamah.

Alisema wizara hiyo ina wajibu wa kuhamasisha, kundezeza na kusimamia ukuzaji viumbe maji ili kuleta maendeleo ya kluchumi ya tawananchi mmoja mmoja na taifa kupitia rasilimali maji inayotoa fursa kushiriki na kunufalka na uchumi wa buluu.

"Azma ya serikali ni kuona fursa za uchumi wa bliuu zinatumika ipasavyo, kuleta ustawi kwa wananchi na kukuza uchumi. Mwaka 2020, sekta hilo imetoa ajira za moja kwa moja kwa wavu wapataan 195,435 na wakuza viumbe maji 30,064 wakati watu zaidi ya milioni 4.5 wanajipatia ki-

pato kutokana na shughuli imbalimbali katika minyororo ya thamani," alisema Dk. Tamatamah.

Aidha, Dk. Tamatamah alisema wafugaji wengi hasa wadogo wanalazimika kutumia mazalii ya kwenye mabwawa yao kama mbegu, hali ambayo haleti tija kutokana na vifaranga hivyo kukosa ubora.

"Kwenye chakula cha samaki, tulikuwa na viwanda II vilivyozaalisho takribani tani 1,000 lakini mahitaji ni tani 27,000. Hapa pia, wafugaji susani wale wadogo wanaishia kutegemea chakula cha asili cha kwenye mabwawa na pia kujitengenezea vyakula vyao na hivyo kuathiri tija," alisema Dk. Tamatamah.

Makamu Mkuu wa chuo hi-

cho, Prof. William Anangisye, alisema wakati uchi jkitaraja kukuza uchumi kupitia uchu-mi wa buluu, ni wakati wa kututua changamoto za upati-kanaji wa chakula cha viumbe hati, vifaranga ili kuwapo usu-gaji wenye tija.

Mbumifu wa Majengo kutoka Wakala wa Majengo Tanazania (TBA), Paschal Kamata alisema mradi huo awamu ya kwanza utakamilika kwa miezi mitano ambao utakuwa na sehemu ya kutotolea na kukuza vifaranga milioni 2.5 vya samaki wenye mapezi.

Pia, alisema mradi huo utakuwa na sehemu ya kuan-gulia mayai ya majongoo bahari na kukuza vifaranga milioni moja patnoja na vifaranga vya kaa milioni moja.

10 NOVEMBER 2020

Wasichana>>Wazazi watakaobainika kusababisha watoto wa kike kukatisha

Wafugaji watakiwa kuacha kutoa rushwa pindi mifugo inapokamatwa shambani

Na IGAMBA LIBONGE, Kilosa

JAMII ya wafugaji wilayani hapa, mkoani Morogoro imetakiwa kuacha utoaji rushwa pindi mifugo yao inaposababisha athari katika mashamba ya wakulima.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Alhaj Majid Mwanga, wakati wa kikao cha viongozi wa wafugaji ambapo ametaka jamii hiyo kujikita zaidi katika kudumisha amani kwa kuhakikisha mifugo yao inakuwa katika uangalizi mzuri ili kuepuka migogoro.

Alisema suala la kudumisha amani ni la kila mmoja, wana wajibu kuhakikisha ulinzi na usalama unatawala katika maeneo yao ili kuifanya Kilosa kuwa sehemu salama kwa wakulima na wafugaji.

"Huwa sijisikii vizuri nikiambiwa kuwa Wilaya ya Kilosa inaongoza kwa migogoro ya wakulima na wafugaji wakati tunajua kabisa kuna vikundi

ya watu wachache kwa kujiona wana fedha hudiriki kutoa rushwa ili kufanikisha malengo yao,"alisema.

Kadhalika, alikemea vikali tabia ya baadhi ya wazazi kuwakatisha masomo wanafunzi kwa sababu mbalimbali na kwamba hatamfumbia macho mzazi na yeyote atakayehusika kumkatisha mwanafunzi masomo kwani watoto wote wana haki ya kupata elimu.

"Kuna baadhi yenu mnajifanya kuendeleza hizo mila potofu za kumzuia mtoto wa kike kwenda shule kwa madai ya kuolewa, sasa ole wake nitakayembaini, nitamchukulia hatua kali za kisheria bila kujali cheo chake ama sura yake,"alisitiza.

Naye, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, Zakhia Fandey, alisitiza jamii hiyo kushiriki kikamilifu katika uwekaji anwani za makazi na kushiriki Sensa ya Watu na makazi ifikapo Agosti mwaka huu.

"Tunawaomba na ninyi mwende mkahamasishe jamii zetu wanashiriki kikamilifu katika shughuli ya anwani za makazi inayoendelea sehemu mbalimbali na pia msisahau kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi ifikapo Agosti mwaka huu, tuache tabia ya kuhamaharma kipindi hicho," alisitiza.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Morogoro, Shambakubwa Longido, aliouomba uongozi wa wilaya kuikumbuka jamii ya wafugaji hususan katika mashamba yaliyofutwa, huku akiomba wafugaji watakaobainika kulishia mifugo katika mashamba na watakaobainika kutopeleka watoto shule, wachukuliwe hatua ili kutoipaka matope jamii hiyo.

"Mkuu tumekusika nasi kama viongozi tutahakikisha hiyo migogoro haitokei tena na pia suala la kuapeleka watoto shule tushaambiana na tunawapeleka, ila tunaomba mtukumbuke jamii yetu katika mashamba mtakayogawa na hii itasaidia kuepusha migogoro, kwani tutakuwa na maeneo yetu ya malisho na pia ya kilimo,"alisema.



Zanzibar Chamber of Commerce executive director Hamad Hamad (3rd-L) and Peak Performance International Tanzania CEO Philemon Kisamo sign an MoU in Dar es Salaam on Monday under which the latter agency will conduct training for ZNCC staff and members. Second left is ZNCC chairman Ali Amour. Photo: Correspondent Miroslav Msalwa



the government has injected 167m/- for the project.

The parliamentary panel has inspected various development projects including mobile communications, installing of postcode address and the national broadband projects.

THE GUARDIAN Page 4

Livestock strategy up for big transformation*

By Guardian Correspondent, Morogoro

THE livestock sector is up for big transformation including 192m/- plan earmarked for implementation aimed at creating bigger projects without government's support.

The remarks were made by the Permanent Secretary in the Livestock and Fisheries ministry (Livestock Division) Dr Tixon Nzunda when addressing officials and workers of the ministry's livestock sector at a meeting held

here at the weekend.

Dr Nzunda stressed that it is their responsibility to continue involving more stakeholders in implementing much bigger plans without the government dependency.

He said the plans aim to make available better livestock breeds, great changes for beefing up water services, livestock folder and other animal's feed, improving livestock health and improvement to livestock extension services to make Tanzania a country without livestock

diseases.

The deputy minister added that other issues for big plans is to strengthen research services and training; adding value to livestock products and improve activities of nation ranches in which the government has provided 470m/- of which 165m/- is set for development projects

He said what he now wants is to see every ranch is self-reliant and called on dormant ranch and auction supervisors to resign, else

they must increase production.

He added: "I know you were being provided with small operational budgets, but beginning the next budget I will beef up support to make sure livestock farms and auction centres have enough working tools."

"I will increase the budgets for auction centres to enable them collect more, and if they fail to do so they will be fired."

"I will never transfer the corrupt, embezzlers or thieves of public funds; I will suspend

them and take legal steps."

He added that he will establish work contracts and workers will be assessed for their performance and provided with incentives for them to work harder as well as for innovation and writing up projects' plans," he added.

Dr Nzunda said the aim of the ministry is to see officials, directors or heads of departments are assessed through open criteria, hence he called on them to change in their work performance and abandon working routinely.

said
its
co-
ns

d
5

8

* DAILY NEWS Page 2.

Tanzania registers first fishing vessel

BY SAULI GILIARD

TANZANIA will for the first time start reaping from its Exclusive Economic Zones (EEZ) after launching a large fishing vessel registered in the country.

Speaking at a launching ceremony held in Dar es Salaam on Monday evening, Minister for Livestock and Fisheries, Mashimba Ndaki said under the deal, licensing revenue will be \$400,000 (approximately 927.6m/-) annually.

After being registered in the country, the Pacific Star fishing vessel, owned by Spanish based Albacora family company, will be sailing under a Tanzanian flag. At the event attended by officials from both Mainland and Isles, the Minister said other benefits of the concluded deal was that Tanzania will get a portion of 300 tonnes of targeted tuna fish and other related species amounting to 100 tonnes per year.

Albacora, which will operate in the country under subsidiary company Pemba Tuna Limited, plans to build a fishing processing factory in the near future, Mr

Ndaki said, adding that the move will give more employment opportunities to Tanzanians.

"Each year, Tanzanian sailors will be trained by the company and service providers will get tenders as well," he added.

On his part, Minister in charge of Blue Economy and Fisheries, Suleiman Masoud Makame said the vessel with a gross tonnage of 4164 will provide great opportunities and experience to Tanzanian sailors.

He said the country has no qualified fishing sailors but since the vessel will do both fishing and navigation; "the country has a good number of specialized navigators who can be employed directly."

Deputy Minister of Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega said the vessel can fish up to over 2,000 tonnes per single trip, saying the installation of processing plants in the country is the ministry's main target.

Chairperson of Bunge's Parliamentary Committee responsible for Agriculture, Livestock and Water, Dr Christine Ishengoma said she was satisfied by the

move which will help the country to explore more opportunities in the industry.

Minister of Livestock and Fisheries, Dr Rashid Tamatamah said one of key strategies of both Mainland and Isles ministries was to attract investors in order to explore more opportunities in the deep sea.

He said the arrival of the vessel was just a beginning and many more are expected, thanks to President Samia Suluhu Hassan's abroad trips which trumpet blue economy opportunities in Tanzania.

Albacora representative Imanol Loinaz said the company has injected around \$24m and said the vessel's crew was composed of 11 Spaniards and the rest were Africans.

According to the Marine Traffic website, the Pacific Star was built in 1990 and it is currently sailing under the flag of Tanzania.

Its carrying capacity is 1905 t DWT and her current draught is reported to be 7 meters. It has length overall (LOA) of 105 meters and her width is 16.8 meters.

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Kwa mara ya kwanza bendera ya Tanzania itapeperuka kwenye meli kubwa ya uvuvi wa bahari kuu.

Hatua hiyo inakuja baada ya Wizarara za Mifugo na Uvuvi za Jamhuri ya Muungano na Mapinduzi Zanzibar kutoa kibali cha uvuvi kwa mwekezaji, Kampuni ya Pemba Turner Limited, iliyoanzishwa nchini na Kampuni ya Albacora ya Hispania.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema wametoa leseni itakayomwezesha mwekezaji huyo kuvua samaki katika ukanda wa bahari kuu nchini na wa kimataifa.

"Meli hii imesajiliwa kwetu na itapeperusha bendera ya Tanzania,

Meli ya kwanza uvuvi wa bahari kuu yaanza kazi

tumeizindua na kuipa leseni kuanza kufanya kazi," alisema na kuongeza kuwa mionganoni mwa manufaa itakayopata nchi, ni kupata samaki tani 300 lengwa aina ya jodari na samaki wasiolengwa tani 100 kila mwaka.

Ndaki alisema manufaa mengine ya uwekezaji ni tozo kwenye leseni iliyoghamariwa Dola 400,000 za Marekani (Sh920 milioni) na itahisshwa kila mwaka, kufundisha wataalamu wa uvuvi wa bahari kuu wawili

kila mwaka na kuajiri Watanzania watano kama mabaharia wa meli hiyo.

Mkurugenzi wa kampuni ya Albacora, Imanol Loinaz alisema meli hiyo ina wataalamu walibobea kwenye uvuvi wa bahari kuu, uwezo mikubwa wa visaa na hisadhi ya samaki pamoja na meli yenye ukubwa wa mita 104, takriban sawa na urefu wa uwani wa soka.

"Tuna uwezo wa kuhifadhi tani

2,400 kwa mkupuo mmoja na kuvua santi kwa siku 30 hadi 45 kabla ya kurudi kwa ajili ya mahitaji," alisema.

Alisema kampuni hiyo itajenga kiwanda cha kuchakata samaki nchini baada ya mwaka mmoja.

Loinaz alitaja mionganoni mwa sababu zilizomsukuma kuwekeza nchini ni mazingira mazuri ya uwekezaji yaliwashawishi kufanya hivyo.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi-Zanzibar, Suleiman Makame alisema wameichunguza kampuni hiyo na wana imani itafanya uvuvi endelevu wenye kufuata sheria za nchi na za kidunia kuhusu masuala ya bahari kuu.

Tani 300

Kiwango cha samaki aina ya jodari kitakachovuliwa katika bahari kuu kwa mwaka.

Tani 2,400

Uwezo wa mell iliyosajili katika kuhifadhi samaki kwa wakati mmoja.